**BUKU LA 17**

Salamu kwa Familia ya Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb,

Asanteni kwa kujitolea kwako kwa wanafunzi wetu. Jana niliadhimisha siku yangu ya 100 na wilaya ya shule na ninajivunia kuwa msimamizi wa Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb. Miezi hii michache iliyopita imenielimisha na kuninyenyekesha na nimejifunza mengi sana kuhusu jamii yetu kutoka kwa washikadau wa ndani na wa nje katika wilaya nzima, huku wakiongoza na kupitia janga hili la kimataifa.

Ninatazamia kushiriki uwezo na nafasi zangu nilizotambua, kuendeleza maono ya DCSD ili kutia moyo jamii yetu ya wanafunzi kufikia ufanisi wao wa kielimu ili wanafunzi wetu wote wazuri na werevu, katika jamii zetu mbalimbali waweze kufikia uwezo wao kamili wa kufanikisha maono yetu kwa hitimu ya Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb.

Asante sana DCSD kwa kuniruhusu kuwa sehemu ya jamii hii na kushirikiana na mabingwa wa ajabu na mashujaa wa usawa wa wilaya hii yenye nguvu ili kutuelekeza Mbele, tunapokuwa tukitiwa moyo, kutimiza na kufanikiwa. Tafadhali tembelea Kona ya Msimamizi kwa maelezo zaidi.




Kama ujuavyo, tulisambaza Fomu ya Nia ya Kurudi Shule mnamo tarehe 9 Oktoba na tumeongezea muda wa makataa hadi tarehe 30 Novemba, 2020. Kwa kukamilisha fomu hii, wazazi/walezi wanaweza kuchagua chaguo lao wanalopendelea kwa kila mtoto. Shule

yetu hutumia data ya ukamilishaji ya Fomu ya Nia ya Kurudi Shule kukusanya maelezo kuhusu familia zinazotaka kurudi muundo mseto au kusalia katika mazingira ya mbali.

**Masomo Mseto (Mchanganyiko wa Masomo ya Ana kwa Ana na ya Mbali):**

- Muundo wa masomo mseto umeundiwa familia zinazohisi sawa kuwarudisha watoto wao kwa mazingira ya masomo ya ana kwa ana yaliyochanganywa na masomo ya mbali.

**Muundo wa Masomo ya Mbali:**

- Muundo wa masomo ya mbali umeundiwa familia ambazo hazihisi vizuri watoto wao wakirudi shuleni katika mazingira ya ana kwa ana kwa wakati huu. Wanafunzi wataendelea kusoma kutoka nyumbani katika mazingira ya mtandaoni yanayotolewa na shule.

Ili kuhakikisha mazingira salama wakati mtoto wako anawasili na kujiandaa kwa masomo yanayoendelea ya mbali, tunahitaji wazazi wote kuwasilisha fomu ya utafiti ya kila mtoto anayehudhuria shule zetu.

Tukikosa kupokea majibu ya utafiti ya mtoto wako, tutachukulia mtoto wako anarudi kusoma katika mazingira mseto. Fomu ya utafiti itafungwa tarehe 20 Novemba, 2020. Tafadhali bofya hapa ili ufanye utafiti:
https://dekalb.co1.qualtrics.com/jfe/form/SV_cO7CQFP10BWfwuF




**Taarifa za COVID-19**

Viwango vya maenezi katika jamii vinaendelea kuongezeka zaidi ya  kigezo cha “Maenezi ya Makubwa” ya visa 100 kwa wakazi 100,000 kwa kipindi cha wiki mbili kama ilivyohesabiwa na Idara ya Afya ya Umma ya Georgia (GDPH). Hadi jana, nambari hii iliyoripotiwa na GDPH ya Kaunti ya DeKalb ni 270. Ili kupata habari mpya kuhusu viwango vya maenezi katika Kaunti ya DeKalb, tafadhali endelea kutembelea: https://dph.georgia.gov/covid-19-daily-status-report. Kuongezeka kwa nambari hizi kunaendelea kusababisha wasiwasi mkubwa na wilaya itaendelea kushiriki vidokezo vya usalama na habari muhimu kulingana na Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC). Kwa hayo, tafadhali angalia video ya muziki ya Wave Them Bows kutoka kwa waalimu na wanafunzi wa bendi wanaohamasisha kuhusu kuwa salama wakati wa janga hili.

Hapa kuna baadhi ya maelezo kuhusu kuvaa barakoa kulingana na CDC:

Funika mdomo na pua lako kwa kutumia barakoa ukiwa karibu na wengine.

- Unaweza kueneza COVID-19 kwa wengine hata kama hauhisi mgonjwa.
- Barakoa imetengenezwa kuwalinda watu wengine iwapo umeambukizwa.

- Kila mtu anapaswa kuvaa barakoa hadharani na karibu na watu ambao hawaishi katika nyumba yako, hasa wakati hatua nyingine za kutokaribiana na watu ni ngumu kudumisha.
  - Barakoa hazipaswi kuvalishwa watoto wadogo chini ya umri wa miaka 2, mtu yeyote mwenye ugumu wa kupumua, au hana fahamu, asiyejiweza au asiyeweza kuondoa barakoa bila usaidizi.
- USITUMIE barakoa uliyokusudiwa mfanyakazi wa afya. Kwa sasa, barakoa za upasuaji na vipumuliaji vya N95 ni bidhaa muhimu ambazo zinapaswa kuhifadhiwa kwa wahudumu wa afya na watu wa kwanza kusaidia.
- Endelea kukaa umbali wa karibu futi 6 kati yako na wengine. Barakoa sio mbadala wa kutogusana na watu.




**<u>Wiki ya Hatua ya 2020 ya Black Lives Matter</u>**

Black Lives Matter katika Wiki ya Hatua ya 2020 ya Shule za DeKalb katika wilaya ilifanikiwa sana. Ninashukuru sana kwa msaada na mawasilisho ya maana kutoka kwa wanenaji wetu wakiwemo Mkubwa wa Polisi wa Kaunti ya DeKalb, Melody Maddox, Hank Stewart wa Wakfu wa Stewart, Dkt. Thomas McBryde, Dkt. Ghody Muhammad kutoka Chuo Kikuu cha Jimbo la Georgia, na Dkt. Haggen kutoka Scholastic. Tutakuwa na video za kushiriki hivi karibuni kwa wanafunzi na familia ambazo huenda zilikosa wiki hii ya himizo. Tafadhali tembelea @dekalbschools kwenye YouTube.

Wakati wa wiki ya BLM, nilistaajabishwa na wanafunzi wetu amba walikuwa wametulia na wazingativu walipokuwa wakiongea kuhusu ukosefu wa haki wa kimbari na madhara yake

duniani na katika jamii zao. Nilifurahia kusikia mipango ya wanafunzi wetu ya kuunda urithi na uthibitisho wao wa kuleta ulimwengu pamoja. Asante kwa Bodi ya Elimu ya DCSD na viongozi wa wilaya waliofanya kazi kwa bidii kufanikisha wiki ya BLM. Tunatazamia kuendelea na vuguvugu hili ili kuwawezesha wanafunzi wetu kutoka jamii mbalimbali. Tafadhali kuwa macho kwa maelezo zaidi kuhusu My Brother's Keeper, mpango wa kitaifa ambao unashughulikia mianya iliyopo ya nafasi ambayo wavulana na vijana wasio wazungu wanakabiliana nayo ili kuhakikisha vijana wote wanaweza kufikia uwezo wao wote. Lengo la DCSD ni kuanzisha sura katika kila moja ya shule 137 za DCSD.

**Kushiriki kwa Jamii**

Asante kwa washikadau wetu wanaohudhuria mikutano ya town hall wiki hii-wafanyakazi wa Ofisi Kuu, Madereva wa Basi, na wa Shule. Mazungumzo haya ni muhimu kwetu tunaoandaa kufungua tena shule na kufanya hivyo kwa usalama.

Tumesheherekea na kuelimisha familia na wazazi wetu wa ajabu wiki hii. Vikao vya Habari vya Mtandaoni na hata pia rasilimali za dijitali, wachuuzi, na zaidi zimetolewa hapa Virtual Parent and Family Empowerment Conference. Asante kwa kushiriki na ufahamu kuwa, kuwezesha familia zetu ili wawaunge mkono wanafunzi wetu ndio kipaumbele chetu! Kwa maelezo zaidi kuhusu Kongamano la Kuwawezesha Wazazi na Familia la Mtandaoni, tafadhali angalia hapa chini.

Mwishowe, ninafuraha kwamba wilaya ina kadirio chanya ya mkopo na tunashukuru kwa juhudi na bidii iliyotekelezwa na wafanyakazi ili kuwezesha hii. Tembelea hapa ili kusoma habari zetu njema: DCSD Receives Positive Rating from Moody's Investors Services.

Natakia familia ya DCSD Mapumziko Mema ya Msimu wa Kupukutika kwa Majani na tafadhali endelea kutembelea tovuti yetu kuhusu taarifa za kufungua shule tena kwenye https://www.dekalbschoolsga.org/school-reopening/.

Shabiki wako wa #1,

Cheryl Watson-Harris